

BIBLIA KWA TASWIRA, AGANO JIPYA KITABU CHA 9
INJILI – Sehemu ya Kenda

MAOMBI

(VISUALIZED BIBLE, Vol 9, N.T. Prayer)

Mwandishi: Ruth H. Greiner

Muchapaji: Frances H. Hertzler

Imegeuzwa kwa Swahili Congo na watumishi wa Mungu katika DR Congo

©1969 Bible Visuals International

PO Box 153, Akron, PA 17501-0153

Telephone: 717-859-1131 Fax: 717-859-4360

www.biblevisuals.org

SOMO 1 – MUFARISAYO NA MUTOZA KODI

Kwa mwalimu kujifunza mbele: Matayo 23:1 – 30; Luka 18:9 – 14; Isaya 40:14 – 19.

Shabaa ya somo: Kujibu maulizo: Maombi ni nini? Tunapaswa omba kwa nani? Nani anaweza kuomba?

Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kujua: Mungu hai wa kweli anasikiaka na kujibu maombi wa wale waliosamehewa zambi zao.

Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kutambua: Hamu ya kuomba Mungu.

Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kufanya: Kuomba na kutubu zambi zao kwa Mungu na kumuomba masamaha.

Somo kwa kifupi: (kuandika ndani ya buku ya mwalimu na za wanafunzi.)

1. Watu wengi wanaomba sanamu.
2. Mufarisayo alikuwa na majivuno.
3. Mutoza kodi aliomba na unyenyekevu mbele ya Mungu.
4. Mungu anasikiaka maombi ya wao wanatubu zambi zao na kuomba masamaha.

Shairi la kujua kwa ufahamu: 1 Petro 3:12 - Kwa maana macho ya Bwana ni juu ya wenye haki, na masikio yake kusikiliza maombi yao.

Maelezo kwa mwalimu:

Kuna mafundisho mengi juu ya maombi katika Neno la Mungu. Sharti tujue mafundisho yale, na kuyazoea katika maisha yetu. Maombi ni faida kubwa sana. Ikiwa wewe, mwalimu, unajua uwezo wa maombi katika maisha yako mwenyewe, masomo haya yatakuwa na faida zaidi kwa wanafunzi wako. Kusudi lako liwe kusaidia wanafunzi kujua kuomba Mungu.

Somo: Nani katikati yetu anaisha kuona mutawala wa inchi? Unakwisha kusemezana naye? Tuseme una hamu sana kuzungumuza naye. Utaweza kuingia mara moja nyumbani mwake na kusema maneno gani unayotaka? Haiwezekani. Yeye ni mwenye kazi nyingi. Ni lazima uwe na sababu kubwa kwa kusema naye. Hata hivi utapaswa kupata ruhusa kwanza.

Kuna mumoja aliye mukubwa sana. Ni Mungu aliye hai, Mwumba wa mbingu na dunia. Yeye ni mukubwa, mwenye hekima na mwenye uwezo. Anakubali watu kufika kwake saa yo yote kuzungumuza naye? Ndiyo. Anawakubali na tena anawaalika kuja kwake. Yeye aliyeumba dunia(miti, majani, maqua, milima, nyama, watu na vitu vyote) anataka watu kusemezana naye. Mungu, anayejua yote na anayeweza yote, ni tayari saa zote kusikiliza wale wanaomwambia mambo yao. Kusemezana na Mungu si nguvu, lakini watu wengi duniani hawajui kitu juu ya maombi ya kweli. Mungu amesimamisha kawaida tunazopaswa kufuata ili maombi yetu yapate majibu.